# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA KUMI NA NNE

**16 FEBRUARI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

### KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 16 FEBRUARI, 2024

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

## III. MASWALI:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

### 225. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali imejipanga vipi kuzuia maafa zaidi katika kipindi hiki cha mvua nyingi zinazonyesha sehemu mbalimbali nchini.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**226. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO (BABATI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Galapo - Babati.

**227. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini utekelezaji wa Mradi wa TACTIC katika Mji wa Tunduma utaanza.

**228. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mpango wa kuhakikisha upatikanaji wa Dawa muhimu, *X-ray, Ultra Sound* na maji kwenye Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali - Mara.

**229. MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Kada ya Askari wa Wanyama Pori katika Halmashauri itaangaliwa kama ilivyo kwa Askari wa TAWA.

**OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

**230. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutangaza miradi mikubwa inayotekelezwa nchini ili Wananchi ikiwemo wa Vijijini waweze kufahamu.

## WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

**231. MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Kijiji cha Ncheli, Matinje na Mwakabuta – Manonga vitapata mawasiliano ya simu.

## WIZARA YA KILIMO:

**232. MHESHIMIWA KATANI AHMADI KATANI (TANDAHIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulipa madeni ya muda mrefu ya Wazabuni wa pembejeo nchini.

**233. MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kilimo nchini.

**WIZARA YA UJENZI:**

**234. MHESHIMIWA SALIM ALAUDIN HASHAM (ULANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga barabara ya lami kutoka Liwale hadi Mahenge ili kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mikoa ya Kusini.

**235. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA (MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, nini tamko la Serikali juu ya ujenzi wa Daraja la Godegode - Mpwapwa.

**WIZARA YA FEDHA:**

**236. MHESHIMIWA NUSRAT SHAABAN HANJE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina Mkakati gani wa kuwajengea uwezo wa Kimamlaka Wakaguzi Wakuu wa Ndani ili kuzuia ubadhirifu na wizi wa mali za Umma.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**237. MHESHIMIWA CHARLES MUGUTA KAJEGE (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itajenga malambo ya kunyweshea Mifugo katika Jimbo la Mwibara.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

## V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

## VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:

**WAZIRI MKUU:**

## VII. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI.

**DODOMA**
**16 FEBRUARI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**